

MPANGO WA UFADHILI WA DHARURA WA KODI YA NYUMBA WA JIMBO LA NEW YORK

UFADHILI



Ufadhili wa hadi dola milioni 35 unatolewa kwa wakaaji wa Jimbo la Erie

Usaidizi unatolewa ili kuwawezesha kulipa salio la kodi ya nyumba la hadi miezi kumi na miwili iliyopita na kulipa mapema kodi ya nyumba kwa miezi mitatu. Pia zipo pesa zinazotolewa ili kulipia salio la bili za matumizi.

MASHARTI YA KUJUMUIISHWA KWENYE MPANGO



Wanaowasilisha maombi sharti watimize masharti yafuatayo:

- (1) Familia sharti zitimize masharti ya mapato (AMI ya asilimia 80).
- (2) Kupungua au kupoteza mapato ya familia kutokana na janga la COVID-19
- (3) Kipaumbele kitapewa katika siku 30 za kwanza za mpango kwa wakaaji wenye mapato ya chini (AMI ya asilimia 50).

JINSI YA KUWASILISHA OMBI



Muda wa kuwasilisha maombi utanza Juni 1, 2021 saa 9 AM

Fomu za kuwasilisha maombi zinapatikana mtandaoni kwenye

<https://otda.ny.gov/erap>



Unaweza kupata usaidizi wa simu siku saba kwa wiki kuanzia saa 8 AM hadi 7 PM kupitia 1-844-NY1-RENT au 1-844-691-7368

HATI ZINAZOHITAJIKA



Wanaowasilisha maombi sharti wawasilishe hati zifuatazo:

- (1) Ithibati ya Utambulisho, (2) Ithibati ya SSN, (3) Ithibati ya upangaji na kodi ya nyumba ya kila mwezi, (4) Ithibati ya Mapato, (5) Ithibati ya Kutoweza Kujikimu kutokana na COVID-19, na (6) Nakala ya Bili ya Gesi au Umeme

Wamiliki wa nyumba wanaweza kuwasilisha maombi kwa niaba ya wapangaji.